

# **WAKALA WA MABASI YAENDAYO HARAKA**



Kumb. Na. AB.23/134/01-J/107

04 Juni 2021

## **TANGAZO LA AJIRA YA MUDA MFUPI**

---

Mtendaji Mkoo wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka, anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenyе sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi kumi na tano (15) kama ilivyobainishwa katika tangazo hili.

### **1. WASIMAMIZI WA MAPATO WASAIDIZI (REVENUE MANAGEMENT ASSISTANT) - NAFASI 09**

#### **1.1. SIFA ZA MWOMBAJI:**

Awe na Elimu ya kidato cha nne (IV) na amehitimу elimu ya ngazi ya cheti katika fani za Uhasibu, Biashara, Manunuzi, Takwimu, Hisabati au nyingine inayofanana na hizo kutoka chuo kinachotambulika na Serikali.

#### **1.2. MAJUKUMU YA KAZI:**

- i. Kufuatilia utararibu wa utaoaji tiketi kwenye mashine (TOMs);
- ii. Kuhakikisha abiria wote wana tiketi;
- iii. Kuhakikisha “*attendants*” wanachana tiketi zilizotumika;
- iv. Kuhakikisha tiketi zilizotumika haziuzwi tena kwenye mfumo;
- v. Kushauri juu ya umuhimu au ulazima wa utoaji wa tiketi nyingi kulingana na uhitaji wa usafiri kwa kituo husika;
- vi. Kuhakikisha kiwango cha makusanyo ya vituo kinaakisi makusanyo yaliyokabidhiwa kwa wasimamizi wa kazi na kuwasilishwa Benki kwa siku husika;
- vii. Kutoa taarifa juu ya viashiria vya ubadhilifu na mambo mengine yasiyo ya kawaida katika ukusanyaji wa nauji; na
- viii. Kufanya kazi nyingine zinazohusiana na usimamizi wa mapato atakazo pangwa na msimamizi.

### **1.3 MSHAHARA:**

Kima cha mshahara kwa mwezi ni hadi shilingi 310,000/=.

## **2. WAHUDUMU WA ABIRIA - NAFASI 06:**

### **2.1. SIFA ZA MWOMBaji:**

Awe na elimu ya kidato cha nne na amehitim u elimu ya ngazi ya cheti katika fani za Afya ya Jamii (Community Health) au fani nyingine inayofanana na hizo kutoka chuo kinachotambulika na Serikali.

### **2.2 . MAJUKUMU YA KAZI:**

- i. Kuwaelekeza abiria sehemu ya kunawa mikono,
- ii. Kuhakikisha abiria wamenawa kabla ya kuingia katika usafiri wanaingia katika usafiri,
- iii. Kutoa taarifa ya mahitaji ya vitendea kazi kwa msimamizi kadiri itakavyohitajika,
- iv. Kusafisha na kujaza maji katika matenki kwa wakati,
- v. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

### **2.3. MSHAHARA:**

Kima cha mshahara kwa mwezi ni hadi shilingi 310,000/= kulingana na mahudhurio.

## **3. MASHARITI YA JUMLA:**

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania,
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa,
- iii. Waombaji wote wawe na umri usiozidi miaka 45,
- iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika,
- v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya kidato cha nne, taaluma, kwa wale waliohitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika waambatanishe vyeti vya mafunzo husika,

- vi. Testimonials”, “Provisional Results”, “Statement of results”, hati matokeo za kidato cha nne (**FORM IV RESULTS SLIPS**) **HAVITAKUBALIWA**,
- vii. Picha moja “Passport size” ya hivi karibuni.
- viii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na Baraza la Mitihani Tanzania - (NECTA),
- ix. Uwasilishaji wa taarifa, nyaraka na sifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

**Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo:-**

Mtendaji Mkuu,  
Wakala Wa Mabasi Yaendayo Haraka,  
S.L.P. 724,  
**DAR ES SALAAM.**

**Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe 13 Juni 2021.**

Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAKUBALIWA**.

Limetolewa na:

**MTENDAJI MKUU  
WAKALA WA MABASI YAENDAYO HARAKA**